**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE**

SHULE YA SEKONDARI MATAMBA,
S. L. P 155,
**MAKETE.**
11 /06/2023

KUMB. NA. MAT/JI/VOL01/04.
MZAZI/MLEZI WA ______________________________
______________________________

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MATAMBA ILIYOPO WILAYA YA MAKETE MKOA WA NJOMBE .**

**1. UTANGULIZI.**
Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha **TANO** 2023 katika shule. hii shule itafunguliwa tarehe **13/08/2023.** Umechaguliwa kujiunga na shule hii kulingana na chaguo lako . Shule ina tahasusi **TATU** kwa sasa, **HKL**, **HGL** na **PCM**. Shule ya Sekondari Matamba ipo wilaya ya **Makete** mkoa wa **Njombe,** shule ipo upande wa kaskazini mashariki kutoka makao makuu ya wilaya. Shule ipo umbali wa **kilomita 70** kutoka wilayani na **kilomita 31 kutoka Chimala- Mbeya**. Kwa wanafunzi wanaotoka nje ya wilaya ya Makete, njia rahisi ya kufika shuleni ni kama ifuatavyo; Kwa wanafunzi wanaotoka mikoa ya kati, kusini, Nyanda za juu kusini, mashariki, Kaskazini, kanda ya ziwa nk. Panda magari yanayokwenda **Mbeya** kisha shuka **Chimala stand ya kati**, hapo utapata mabasi yanayofika moja kwa moja **Matamba** nauli ni **Tsh. 5000** tu. Kwa wale wanaotoka, mikoa ya,Rukwa, Songwe, Katavi Nk. Panda magari yanayokwenda Mbeya, shuka stand ya **Nanenane-Mbeya mjini** hapo ulizia mabasi yanayokwenda Matamba(**Uwanji**) moja kwa moja kwa nauli ya Tsh **9000** tu.

**Tafadhali sana**: uvunjaji wa kanuni na taratibu za Shule hautavumiliwa. Ni **marufuku** mwanafunzi **kumiliki simu** ya mkononi, mwanafunzi akipatikana na simu **atarudishwa nyumbani** na **simu itavunjwa**. Tafadhali soma maelekezo yaliyoambatanishwa na barua hii na uyatekeleze, kisha jaza fomu zilizoambatanishwa na kuziwasilisha shuleni.

**2. MAHITAJI MUHIMU**
Yafuatayo ni maagizo/mahitaji/michango na vifaa muhimu ambavyo ni lazima uje navyo siku unapokuja hapa shuleni.
**FEDHA**

(i) Mchango wa Taaluma Tsh 20,000/=
(ii) Ukarabati wa samani Tsh 15,000/=
(iii) Wapishi, ulinzi na vibarua wengine Tsh 30,000/=
(iv) Nembo ya shule 5000/=
(v) Kitambulisho Tsh 5000/=
(vi) Fedha ya tahadhari Tsh 5,000/= (haitarejeshwa)

**MUHIMU.** ***michango kwa mwaka mzima ni Tsh 80,000/= Michango yote inatakiwa kulipwa awamu ya kwanza tu.***
***MUHIMU.*** FEDHA HIZI ZOTE ZIINGIZWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE ***60401600940 MATAMBA SEKONDARY SCHOOL EK/AC NMB.*** Andika jina la mwanafunzi unayemlipia na orodhesha vitu vilivyolipiwa. Hatutapokea fedha mkononi, njoo na **BPS** hapa shuleni ili ukatiwe risiti.

### 3. SARE ZA SHULE (WAVULANA) TU

(i) Suruali mbili, moja kijani kibichi na nyingine Dark Blue. Suruali iwe na mshono wa Turn up, celebration na mifuko mitatu mmoja nyuma na miwili mbele.

(ii) Mashati mawili rangi nyeupe(tetron) mikono mirefu yanayoweza kuchomekwa ndani ya suruali.

(iii) Masweta mawili, moja rangi ya kijani kibichi na lingine Dark Blue.

(iv) Tshirt yenye nembo ya shule rangi ya blue.

(v) Suruali za Khaki mbili. Moja aivae siku anakuja kuripoti. Jambo la kuzingatia ni kwamba nguo za nyumbani hatakiwi kuja nazo kabisa( tafadhali mzazi zingatia hilo) pia zingatia mshono.

(vi) Viatu rangi nyeusi vya kamba na kisigino kikubwa, jozi mbili.

(vii) Soksi jozi mbili rangi nyeusi.

(viii) Track suit moja rangi ya blue itavaliwa michezoni na wakati wa prepo (night preparation).

(ix) Vifaa vya michezo/aje na jezi ya blue na viatu vya michezo(raba) nk.

(x) Tai rangi ya kijani kibichi moja na Dark blue moja inayofanana na suruali hapo juu.

(xi) Lab coat kwaajili ya masomo ya vitendo kwa wanafunzi wa PCM.

(xii) Koti moja zito jeusi lisilo na maandishi kwaajili ya kuvaa mwanafunzi wakati wa jioni

**NB:Si jukumu la shule kushona sare za shule za mwanafunzi; mwanafunzi husika ataelekezwa kwa mtu/fundi aliteuliwa na shule kwa kazi hiyo. Utaratibu huu umewekwa ili wanafunzi wawe na sare zinazofanana kwa rangi na mshono. Kama mzazi utaamua kumshonea mwenyewe, rangi au mshono ukawa tofauti , mzazi utalazimika kumshonea sare nyingine upya.**

### 4. VIFAA VYA BWENI (KWA WAVULANA)

a) Godoro la sponji inchi $2\frac{1}{2}$ aje nalo au kama usafirishaji ni shida aje na fedha atanunua kwenye maduka jirani na shule.

b) Mashuka mawili rangi ya light blue (maji ya bahari) na pink),

c) Blanketi zito moja, mto na foronya yake rangi blue

d) Taulo.

e) Vyombo vya kulia chakula: Sahani, kijiko, kikombe.

f) Mafuta ya kupaka, Toilet paper, dawa ya meno, miswaki, sabuni za kufulia na kuoge.

g) Ndoo mbili za lita 10 zenye mifuniko, ndoo moja atakabidhi shule na nyingine kwa ajili ya matumizi yake binafsi.

h) Tranka moja (01) na kufuri imara la kuwekea vifaa vyake binafsi ikiwa ni pamoja na nguo zake. Usije na begi ambalo ni rahisi kuchanika.

### 5. MAWASILIANO NA SHULE

(1) Barua; S. L. P 155, Makete- Njombe

(2) 0766 327 130 Mkuu wa Shule

(3) 0768 302 749 Makamu wa Mkuu wa shule

(4) 0766 869 113 Mwandamizi Taaluma

(5) 0755 553956/0688 632 126 mwandamizi malezi

**0769642817 HII NI NAMBA YA SHULE,NI MUHIMU SANA KILA MZAZI AWE NAYO KWA SABABU MAWASILIANO YOTE YA MWANAFUNZI NA MZAZI YATAFANYIKA KWA NAMBA HII NA SIO VINGINEVYO.MZAZI HAURUHUSIWI KUTUMIA SIMU NYINYINE ZAIDI YA HII KWA**

**PHYSICS**

a) Chand S. ( ) Conceptual Physics for Class XI and XII
b) **NELKON AND PARKER**
c) **T.I.E ( ) Physics for Advanced Level Secondary Schools, Students Book Form Five.**
d) **T.I.E ( ) Physics for Advanced Level Secondary Schools, Students Book Form Six**
e) **Roger Muncaster ( ) A-Level Physics.**

**ADVANCED MATH**

a) Septine I .S ( ) Advanced Mathematics
b) Mayombya P. L ( ) Conceptual Advanced Mathematics for Form Five and Six
c) Shayo ( ) Advanced Mathematics.
d) Tranter & Laube ( ) Advanced Mathematics.
e) Back House ( ) Pure Mathematics Vol 1
f) Back House ( ) Pure Mathematics Vol 2
g) Chand S. ( ) A Level Mathematics Volume I and II

## 8. MAELEKEZO MUHIMU

a) Baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kuwatelekeza watoto wao bila kuwapa mahitaji muhimu na fedha za matumizi wakiwa shuleni hivyo kuleta usumbufu kwa shule na kuwafanya wanafunzi kugeuka omba omba wakifikiri shule ina utaratibu wa kuwa na fedha. Kitu ambacho si kweli. Ni jukumu lako mzazi/mlezi wa mwanafunzi kumpatia fedha za mahitaji mwanao kupitia simu ya shule au akaunti yake ya Benki.

b) Baadhi ya wanafunzi wamekuwa na tabia ya kukataa, kufanya kazi za nje kama usafi wa bweni, kufyeka n.k. shule haitamvumilia mwanafunzi yeyote atakayeonesha tabia hiyo. Shule haitakuwa na huruma na mwanafunzi wa aina hii. Mwanafunzi lazima afundishwe Elimu ya kujitegemea. Na hii ndio sera ya Taifa letu, atafanya kazi zote za shule.

c) **SIMU**. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu awapo shuleni ikiwa ni pamoja na vifaa vya muziki na kamera. Mawasiliano yote ni kupitia shule kwa namba tulizoorodhesha. Ni vizuri ukalielewa hili, kwani shule haitakuwa na huruma katika hili.

d) Usifike bwenini bila kuripoti Ofisi ya Mkuu wa Shule au Makamu wa Mkuu wa shule.

e) Bank Paying Slips (BPS) ziwasilishwe kwa mhasibu wa shule hapa shuleni. Hakikisha unapewa stakabadhi. Ahadi za kulipa baadae hazitasikilizwa.

f) Vazi la shule ni lazima livaliwe wakati wote wa masomo na kwenye shughuli rasmi. Mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi kabisa uwapo shuleni.

g) Maagizo ya fedha(karo na michango yote) na mahitaji yote muhimu vitakaguliwa mara tu mwanafunzi atakapofika kujiunga na shule hii. Visipokamilika mwanafunzi atarudishwa nyumbani kuvifuata.

h) Ni marufuku kuja na kofia, pete na mapambo mengine au mitindo isiyofaa ya kunyoa nywele.

i) Hairuhusiwi kufuga nywele na ndevu, muda wote nywele ziwe fupi.

j) Ikiwezekana mfungulie mwanao akaunti ya Benki, au atafungua aikwa hapa shuleni kwa kushirikiana na Benki za NMB na CRDB Makete.

k) Hatutaruhusu mwanafunzi kubaki wakati wa likizo, hakikisha mzazi unatuma nauli mapema, sababu chakula cha kuwalisha wanafunzi wakati wa likizo hakipo.

## 9. AFYA

Unatakiwa kupima afya yako kabla ya kuripoti shuleni. Fomu maalumu imeambatanishwa kwa ajili hiyo na utatakiwa kukabidhi fomu hiyo iliyokamilika mara tu ufikapo shuleni.

Kama unamatatizo ya muda mrefu ya kiafya toa taarifa ufikapo shuleni. Vyeti vya tatizo lako ni lazima uje navyo kuthibitisha hali yako. Shule haina uwezo wa kutoa chakula maalumu cha wagonjwa wa kudumu. Pia shule haitavumilia mwanafunzi anayejisingizia ugonjwa kwa sababu zake binafsi. Fomu ya daktari itatumika katika maamuzi yote.

USHAIRI

a) Kimbunga – Haji Gora
b) Fungate ya Uhuru
c) Mapenzi Bora – Shaban Robert
d) Chungu Tamu – T. Mvungi

RIWAYA

a) Mfadhili – Hussein Tuwa
b) Kufikirika – Shabani Robert
c) Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile
d) Vuta n'kuvute – Shafi A. Shafi

TAMTHILIYA

a) Morani – Emmanuel Mbogo
b) Kivuli Kinaishi – Said Mohamed
c) Nguzo Mama – Penina Mhando
d) Kwenye Ukingo wa Thim

KISWAHILI I

a) Saluhaya (2010) Nadharia ya Lugha STC DSM- Tanzania
b) Masebo J.A (2012) Nadharia ya Kiswahili kidato cha 5 na 6.

**GENERAL STUDIES**

a) Nyambari N. (2009) Advanced Level General Studies.
b) Kamili Z. ( 2017) General Studies Alive
c) Bigirwamungu J & Deogratias (2019) Understanding General Studies for Advanced Level 5th and 6th Edition.
d) Mwaipaja M. (2020) General Studies for Form Five and Six

**GEOGRAPHY**

a) Clarke J.T (Ed) (1975) An Advanced Geography of Africa.
b) Sibuku K.K & Isengum (1986) Outline of Soil Science.
c) Msabila D.T (2003) Success in Geography Climatology.
d) J.W.N & Salosu F.K (    ) The Essential Of Practical Geography Advanced Level Form 5 and 6, Questions with Answers.

**HISTORY I & II**

a) Oxford (2011) Advanced Learners. History Form 5 and 6. Oxford university press(T) Ltd. Dar es salaam
b) Kamili Z (2015) Advanced level. History part One alive. Kot publishers
c) Walter Rodney (1976) How Europe Underdeveloped Africa. TPH. Dar es Salaam.
d) Perry Davis (1985) History of the World. Houghton Milton Company Washington
e) Ben W. (    ) Modern World History Second Edition.
f) Ellis E. (    ) World History Modern Era.
g) Yasin S. (    ) Advanced History 1 and 2.
h) Shibitali (    ) Advanced History 1 and 2.

**CHEMISTRY**

a) Chand S. (    ) Conceptual Chemistry for Class XI and XII
b) T.I.E (    ) Advanced level Inorganic Chemistry Part I&II
c) Advanced Chemisty Review
d) Ramsden E.M (    ) A. Level Chemistry, 4th edition
e) Ngaiza (    ) Organic Chemistry.

**MAWASILIANO YA WANAFUNZI NA MZAZI. UTARATIBU WA KUTUMIA SIMU ZA WALIMU HAURUHUSIWI KABISA.**

Kwa ufafanuzi zaidi juu ya mambo yanayohusu shule, namna ya kufika, mahitaji wasiliana na namba hizo hapo juu utapata msaada na maelezo ya kina.

**6. VIFAA VYA USAFI**

(i) Brush ngumu 01

(ii) Jembe moja lenye mpini

(iii) Soft bloom 01

(iv) Kwanja 01

**7. VIFAA VYA KITAALUMA**

(i) Daftari counter books 10 kwa ajili ya notes za masomo yake

(ii) Begi la kubebea daftari ni lazima kuwa nalo.

(iii) Advanced Dictionary kwa wote (ni muhimu sana kwa wanafunzi wa Kiingereza kwani ni sehemu ya somo)

(iv) Wanaochukua tahasusi yenye Kiswahili waje na Kamusi na wenye Jiografia waje na Atlas.

(v) Scientific Calculator F(x) 991 kwa wanafunzi wanasoma PCM na somo la Jiografia.

(vi) **REAM (A4) mbili (02) za karatasi kwa mwaka. (ni muhimu sana)**

**VITABU VINAVYOTUMIKA**

ENGLISH LANGUAGE

a) James J(2012) Advanced English Language, form Six and Form Five. Oxford University Press
b) Asheri N (2010) Advanced Level English Second Edition. Good book publisher, Dar es Salaam.
c) Mnyawi F ( )
d) T.I.E (2022) English for Advanced Secondary Schools Student's Book, Form 5 and 6. Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam

**(and any useful book you would come across)***

**Advanced literature** NOVELS

a) A Man of the People – Chinua Achebe
b) The Rape of the Pearl – Magala Nyajo

PLAYS

a) An Enemy of the People – Henrick Ibsen
b) The Bride – Austin Bukenya

POETRY

a) Selected Poems – Institute of Education
b) The Wonderful surgeon and other poems – Charles Mloka

**VITABU VYA KISWAHILI**

KISWAHILI II

a) JPD Company (2008) Kiswahili II kidato cha 5 na 6, General Supplies Ltd. Dar es salaam.
b) J.A Masebo (2011) Nadharia ya Fasihi kidato cha 5 na 6. Nyambari Nyangwine

ZIADA

a) Kaptura la Max – Kezirahabi
b) Rosa Mistika – Kezirahabi
c) Mirathi ya Hatari-
d) Moto wa Ngome ya Mianzi } Mianzi Ngoma ya mianzi

***Mwanafuzni aje na Bima ya Afya kama anayo, ambaye hana anashauriwa kujiunga kwenye Bima za Kikaya CHF kwa mwaka.( NI LAZIMA AWE NAYO ILI KUONDOA USUMBUFU)***

**10. UHURU WA KUABUDU**

Utaruhusiwa kuabudu kulingana na dini yako ila kwa kufuata sheria, ratiba na taratibu za shule na za nchi ingawa tabia ya kubughudhi wengine haitavumiliwa. Ukitaka kubadili dini ukiwa shule utatakiwa kuleta uthibitisho wa barua toka kwa wazazi wako. Shule ni ya mchanganyiko pia kumbuka serikali haina dini hivyo shule haitakubali kuleta taratibu Fulani ili kubughudhi wengine.

**11. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

12.a)Kuiba

b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 (utoro) bila taarifa.

c) Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzio, walezi na wakubwa

d) Kugoma na kuhamasisha mgomo

e) Kupigana na mwanafunzi au kumpiga mwalimu

f) Uasherati na kujihusisha na mapenzi shuleni.

g) Kuoa au kuolewa

h) Kutembelea majumba ya starehe, guest house, au hosteli za wasichana

i) Ulevi/matumizi ya dawa za kulevya au kukutwa navyo

j) Kudharau bendera na wimbo wa taifa.

k) Kumiliki simu ya mkononi shuleni.

l) Kuharibu mali za shule kwa makusudi au kuuza mali za shule

m)Kugoma kufanya kazi halali za shule ambazo ni kwa manufaa ya mwanafunzi awapo shuleni.

n) Kuondoka shule kabla ya muda halali wa serikali na kutohudhuria Baraza la Kufingia shule.

o) Kujihusisha na mapenzi ya jinsi moja.

____________________________

**SHUKURU JOSHUA SANGA**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
MATAMBA SEKONDARI
S. L. P. 155-MAKETE

**NAKALA;**
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,
S. L. P 6,
**MAKETE.**

***NB. Matibabu ya mtoto ni jukumu la mzazi na si la shule.***

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

MATAMBA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 155
MAKETE- NJOMBE
DATE..........................

TO
THE MEDICAL OFFICER.
........................................ ........................................

PART A:

Mr/Mrs/Miss.............................................................................................

Please examine the above named pupil as his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories.

1. Hemoglobin ..........................................................................
2. P.V bleeding ..........................................................................
3. Eye sight ..........................................................................
4. Blood pressure ..........................................................................
5. Urine for sugar ..........................................................................
6. Stool for routine examination ..........................................................................
7. Asthma ..........................................................................
8. Skin disease ..........................................................................
9. Leprosy ..........................................................................
10. Epilepsy ..........................................................................
11. Any deformity ..........................................................................
12. Pulmonary tuberculosis ..........................................................................
13. Neurosis ..........................................................................
14. Venereal diseases ..........................................................................
15. Other serious Diseases ..........................................................................
16. Pregnancy ..........................................................................
17. Covid 19 test ..........................................................................

Thank you
..............................
SHUKURU J.SANGA
THE HEADMASTER

MKUU WA SHULE
MATAMBA SEKONDARI
S. L. P. 155-MAKETE

PART B

(To be completed by the government Medical Officer)

1. I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for full schooling.
2. OTHER COMMENTS

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

Date______________________ Name and signature______________________

Designation______________________ Official stamp ______________________

Form N0.2

## AHADI YA MWANAFUNZI

SHULE YA SEKONDARI
MATAMBA
S.L.P 155
MAKETE-NJOMBE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MATAMBA
S.L.P 155
MAKETE NJOMBE

Mimi_______________________________________ NINAKUBALI/SIKUBALI kuipokea nafasi hii ya kujiunga na shule ya sekondari Matamba kidato cha______________ mwaka__________________ Naahidi kufuata sheria ,kanuni na maelekezo halali nitakayopewa na Uongozi wa shule.Nitashirikiana na Jumuia nzima ya shule ili kuleta UMOJA,AMANI NA MSHIKAMANO na hatimae kuinua maendeleo ya shule na Taifa kwa ujumla katika Nyanja mbalimbali.

Naamini nidhamu ndiyo msingi wa mafanikio yote.

.................................................  ..............................

SAHIHI YA MWANAFUNZI  TAREHE

.................................................  .......................................

JINA NA SAHIHI YA MZAZI/MLEZI  TAREHE

---

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi........................................................mzazi/mlezi wa mwanafunzi.........................................................ninaahidi kumhudumia na kumpa mahitaji yote yanayotakiwa shuleni.Nitashirikiana na Uongozi wa shule kumlea kwa kufuata maadili ya jamii ya taifa hili. Mwanangu shuleni alelewe katika maadili ya dini ya.........................................................(.Dhehebu kwa wakristo)la..................................

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI..................................................................................

mkoa.........................................................wilaya............................................................ ..................................

..............................

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI  TAREHE